TANGAZO LA SERIKALI Na. 50R la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE HUDUMA ZA USHAURI ELEKEZI WA KIHANDISI NA UJENZI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA MASHAMBA YA MIWA, UKAMUAJI WA MIWA NA UFUNGASHAJI WA SUKARI WA KAMPUNI YA MUFINDI PAPER MILLS YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Huduma za Ushauri Elekezi wa Kihandisi na Ujenzi katika Mradi wa Uanzishaji wa Mashamba ya Miwa, Ukamuaji wa Miwa na Ufungashaji wa Sukari wa Kampuni ya Mufindi Paper Mills ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 3 Julai, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Mufindi Paper Mills kwenye huduma za ushauri elekezi za kihandisi na ujenzi katika Mradi wa Uanzishaji wa Mashamba ya Miwa, Ukamuaji wa Miwa na Ufungashaji wa Sukari inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 31 Mei, 2028 kwa mujibu wa kipengele cha 3.4 cha mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Mufindi Papers Mills na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*